



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO

MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA  
CHUO CHA USAFIRI WA ANGA



## **MAFUNZO YA URUSHAJI WA NDEGE ZISIZOKUWA NA RUBANI AWAMU YA TATU KANDA YA KASKAZINI-ARUSHA KUANZIA 15 FEBRUARI HADI 12 MACHI 2021**



Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (Civil Aviation Training Centre) kilichopo jengo la zamani la uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) “terminal one” anawatangazia mafunzo ya ndege zisizokuwa na rubani (Drones Pilot Training) awamu ya tatu yatakayofanyika kuanzia tarehe 15 Februari 2021 hadi 12 Machi 2021 (wiki 4). Mafunzo haya yataendeshwa kwa kushirikiana cha Chuo cha Prowings Training Limited toka Afrika Kusini.

Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne au zaidi, ajue kusoma na kuandika kiingereza na pia awe na umri kuanzia miaka 21.

Awamu hii ya tatu mafunzo yatafanyika Arusha katika chuo cha Nelson Mandela African Institute of Science and Technology (NM-AIST). Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa masaa sita (6) kila siku kuanzia saa mbili na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri. Mafunzo yataendeshwa kwa nadharia darasani na kwa vitendo katika viwanja vya NM-AIST.

Kinadharia washiriki watajifunza:

- Sheria za usafiri wa anga
- Uelewa wa ndege zisizokuwa na rubani
- Uwezo wa ndege, mipango na upangaji wa mizigo
- Hali za kiutendaji zinazoweza kuhatarisha shughuli za urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani
- Hali ya hewa
- Mifumo ya ndege zisizokuwa na rubani inayoiwezesha kupaa angani
- Taratibu na shughuli za urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani
- Kanuni za urukaji wa ndege zisizokuwa na rubani
- Mawasiliano ya sauti kwa wana anga

Ada: 1,980,000/= ambayo itajumuisha chai ya saa nne, chakula cha mchana na vifaa vya kufundishia.

Baada ya mafunzo wahitimu watatunukiwa vyeti vitakavyowawezesha kuomba leseni ya urushaji wa ndege hizo kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

Fomu za maombi zinapatikana Chuoni au unaweza kupakua na kujaza kutoka kwenye tovuti ya Chuo cha Usafiri wa Anga [www.catc.ac.tz](http://www.catc.ac.tz).

**Tafadhali tuma maombi yako mapema na utajibiwa ndani ya siku moja na utapewa taratibu za malipo kupitia mawasiliano yako utakayotuachia.**

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

Mkuu wa Chuo, simu na: +255 715 527575, Barua pepe: [aristid.kanje@tcaa.go.tz](mailto:aristid.kanje@tcaa.go.tz) au

Mratibu wa mafunzo, simu na: +255764 555054, Barua pepe: [hamis.kisesa@tcaa.go.tz](mailto:hamis.kisesa@tcaa.go.tz)

**Imetolewa na:**

**Mkuu wa Chuo,**

**Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC),**

**Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) Terminal one,**

**S.L.P. 18157,**

**DAR ES SALAAM.**